*Kioo cha Lugha, Juz. 20 (2), 150-164*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i2.1

# Uolezi[1] katika Kujenga Utambulisho wa Wahusika katika Riwaya za *Nagona* na *Mzingile* za Euphrase Kezilahabi

*Leonard Flavian Ilomo*[2]

**Ikisiri**

Uolezi ni mbinu muhimu ya kinaratolojia katika kueleza mtazamo au mwono. Hii ni mbinu inayotofautisha baina ya nani anaona na nani anasimulia. Kimsingi, mbinu hii hutumika katika kujenga uelewa na mtazamo juu ya masuala mbalimbali katika matini simulizi (Flavian, 2021). Dhima mojawapo ya mbinu hii inayojitokeza kwa uwazi ni kumfanya msomaji aone jambo fulani na kisha achukue mtazamo ambao utamwezesha kuyatazama mambo kwa mwelekeo fulani. Hata hivyo, kutokana na uchambuzi wa riwaya za *Nagona* (Kezilahabi, 1990; 2011) na *Mzingile* (Kezilahabi, 1991; 2011) ambao tumeufanya katika makala hii, uolezi unaonekana kutumika kujenga utambulisho wa wahusika. Katika makala hii wahusika ambao wameshughulikiwa ni Paa kutoka katika riwaya ya *Nagona* na Mzee kutoka katika riwaya ya *Mzingile*. Uchambuzi umeonesha kuwa utambulisho wa wahusika, Paa na Mzee, umejengwa kupitia uolezi wa mazingira yanayowazunguka, mwonekano wao pamoja na kupitia fikra za wahusika wengine. Kwa ujumla, makala hii imebainisha kuwa uolezi, zaidi ya kuwa mbinu ya kujenga mtazamo kinaratolojia, pia umetumika kujenga utambulisho wa wahusika katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inashughulikia uolezi wa utambulisho wa wahusika katika riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Nagona* (Kezilahabi, 1990; 2011) na *Mzingile* (1991; 2011).[3] Uolezi ulioshughulikiwa ni ule unaowahusu mhusika ‘Paa’ kutoka katika *Nagona* na mhusika “Mzee” kutoka katika *Mzingile*. Wahusika hawa wameshughulikiwa kwa sababu ni wenye kutatiza na ndio ambao, katika riwaya hizi, wanaonekana kuwashughulisha wahusika wengine. Mathalani, katika riwaya ya *Nagona*, nguli wa riwaya hii yupo safarini kumsaka ‘Paa’ ambaye amekuwa akisakwa kwa karne nyingi. Aidha, katika *Mzingile*, naye nguli wa riwaya yupo safarini kumsaka ‘Mzee’ ambaye ni lazima apatikane ili jamii ipate ufumbuzi.

---

[1] Istilahi hii imetumika kurejelea istilahi ya *focalisation* katika Kiingereza.

[2] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
Baruapepe: ilomo.leonard@udsm.ac.tz au leonardilomo@gmail.com

[3] Riwaya ya *Nagona* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1990 na ya *Mzingile* mwaka 1991. Katika makala hii yametumika matoleo ya mwaka 2011.

Safari hizi, ingawa zinaonekana kuwa ni za kuwatafuta wahusika hao katika kiwango cha kwanza, katika kiwango kingine ni safari za kusaka 'ujuzi na ukweli' katika *Nagona* (Diegner, 2005), na kusaka 'uhuru na maana ya maisha' katika *Mzingile*, mambo ambayo yanaonekana kuwa kwa sasa hayapo kutokana na kila kitu kuhusishwa na Mzee. Kwa hiyo, katika makala hii tumeshughulikia namna uolezi ulivyosawiri mtazamo wa mwandishi dokezi[4] juu ya wahusika na namna utambulisho wa wahusika hao unavyojidhihirisha.

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya za *Nagona* na *Mzingile*

Kipengele hiki kinatoa muhtasari wa riwaya za *Nagona* na *Mzingile*. Riwaya hizi, ingawa zimeshughulikiwa na wataalamu wengi kwa namna tofauti, bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzichunguza kwa sababu, kama ilivyo jina la riwaya ya *Mzingile*, riwaya hizi ni mzingile na kwa hiyo, kila msomaji anaweza kuichunguza kwa jicho lake. Hivyo, kabla ya kuzichambua, katika kipengele hiki kumewasilishwa muhtasari wa riwaya hizo ili kujenga uelewa wa jumla.

### 2.1 *Nagona*

Riwaya hii ilichapishwa mnamo mwaka 1990. Inahusu motifu ya safari ya nguli wa kiume asiyejina katika nyika na tajiriba zake zisizo za kawaida. Katika safari yake anakutana na wanafalsafa mashuhuri, miongoni mwao wakiwa Marx, Nietzche na Freud ambao wamekaa katika duara wakizungumza na roho zao ambazo wamezitemea katika viganja vyao. Kisha nguli wa riwaya hii anagundua kuhusu kuwapo kwa paa wa ajabu na anaamua kumfuatilia kwa kuangalia nyayo zake. Ili kumkamata anapaswa kuhimili majukumu ambayo yanaonekana kutokuwa na suluhu. Ingawa majukumu hayo yanaonekana kuwa magumu, nguli huyo anafanikiwa kumpata paa kwa kusaidiwa na wazee wanne ambao wana uwezo wa ajabu. Baada ya kumpata paa ambaye anaonekana kuwa ni mwanamke mzuri, nguli anashindwa kumtunza na paa anamtoroka.

Katika sura ya nane kunafanyika maungamo ambayo kwa hakika ni vigumu kueleweka kama yanafanywa na nguli au vinginevyo. Mhusika anaonekana kuungama dhambi za karne mbili zilizopita ambazo wanadamu wamezitenda, anaungama dhambi hizo kwa Padri. Kisha katika riwaya hii inaonekana kuna 'ngoma ya ungamo kuu' inayosubiriwa. Ngoma inapowadia, makundi mbalimbali kama vile ya wanafalsafa, wanasaikolojia, wanamapinduzi na vichaa yanajitokeza kushindana. Nguli wa riwaya hii anashiriki ngoma hii akiwa na kundi la vichaa. Mwisho wa riwaya hii msichana aitwaye 'Nagona' anazaliwa na nguli anamfuata.

[4] Istilahi hii imetumika kurejelea istilahi ya *implied author* katika Kiingereza.

**2.2 *Mzingile***

Riwaya hii ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1991. Simulizi inaanza na kisasili cha kuzaliwa Mzee ambaye wanamwita Kakulu. Riwaya hii ni mwendelezo wa riwaya ya *Nagona*. Kama ilivyo *Nagona*, riwaya hii nayo inahusu motifu ya safari ya shujaa asiye na jina. Shujaa huyu anajiita Mimi na ni miongoni mwa wasimulizi wa riwaya hii. Huyu Mimi anatumwa kupeleka ujumbe wa kifo cha Mkombozi wa pili kwa babaye anayeitwa Mzee. Lakini safari yake ya kumtamfuta Mzee inampeleka pia katika kutafuta kiini na maana ya maisha. Mimi anafanikiwa kumpata Mzee katika kijumba chake juu ya mlima na kufanya naye mazungumzo. Hata hivyo, Mimi anashindwa kumshawishi Mzee kuhudhuria mazishi ya mwanawe. Kutokana na hali hii, Mimi anaamua kurudi na safari yake inampeleka katika kutafuta majibu ya maswali ambayo hajaulizwa. Inamchukua Mimi karne nyingi kufika kijijini kwake. Anapofika anagundua kuwa kijiji kimeharibiwa na mabomu ya nyuklia na kubaki magofu.

Anapoingia katika nyumba yake iliyoharibiwa, Mimi anamkuta Mzee na mazungumzo yanaendelea. Baada ya kitambo kirefu mvua inaanza kunyesha na uoto unarudi katika hali yake. Katika kipindi hiki mwanamke anajitokeza kimaajabu na kumuongoza Mimi kuelekea ulimwengu mpya na kumuacha Mzee ambaye baadaye anatoweka. Mimi na Mwanamke wanaishi pamoja na kuanzisha ulimwengu mpya. Wote wanaonekana kujua makosa yaliyofanyika zamani. Ili kuepukana na makosa hayo hapo baadaye, wanaamua kujenga ulimwengu mpya bila kutumia maarifa yaliyopo.

**3.0 Dhana ya Uolezi katika Nadharia ya Naratolojia**

Uolezi ni zana muhimu katika uchambuzi wa matini. Wafula (2011) akimrejelea Chatman (1978) anasema kuwa uolezi ni dhana inayochukuliwa kama mbinu ya kiusimulizi. Mbinu hii hutumiwa na mwandishi ili kuiwasilisha hadithi katika matini kutokea pembe fulani. Pembe hiyo ya kuyatazama mambo huchaguliwa na mwandishi ili kuwasilisha mawazo mbalimbali katika bunilizi yake. Katika Nadharia ya Usimulizi, baadhi ya wanazuoni, wanairejelea dhana ya uolezi kama mtazamo (Jahn, 1996; Rimmon-Kenan, 2002; Bal, 2009). Hata hivyo, wanazuoni hawa wanaeleza kuwa 'mtazamo' ni dhana jumuishi. Ujumuishi wa dhana ya mtazamo unatokana na sababu inayotolewa na Bal (2009) kuwa dhana hiyo ya mtazamo "haitofautishi kati ya wanaoona na wanaosimulia" (uk. 146). Kwa hiyo, Nadharia ya Naratolojia imetofautisha kati ya muolaji na msimulizi kwa sababu wananadharia wa mwanzo waliwaweka mawakala hao katika dhana ya mtazamo. Hivyo, ili kutofautisha baina ya nani anazungumza na nani anaona, Genette (1980) alitumia dhana ya uolezi akimaanisha nani anaona nini. Uolezi ni "uhusiano kati ya taarifa ya msimulizi na mawazo ya mhusika ambayo msimulizi anaweza asiyafikie au akayafikia kiasi kidogo au akayafikia pasipo kizuizi" (Nelles, 1990:368). Uhusiano huu upo "baina ya kuona, wakala anayeona na kile kinachoonwa" (Bal, 2009:149). Wazo linalodhihirishwa ni kuwa katika hadithi

kuna msimulizi anayesimulia kile ambacho muolaji anakiona kikitendwa na mtenda. Uolezi huathiriwa na utambuzi wa mtu anayeola. Utambuzi wa muolaji kuhusu kiolwa fulani hutegemea mambo au sababu kadhaa. Chambilecho Bal (2009):

> *Perception depends on so many factors that striving for objectivity is pointless. To mention only a few factors: one's position with respect to the perceived object, the fall of the light, the distance, previous knowledge, psychological attitude towards the object; all this and more affects the picture one forms and passes on to others* (uk. 145).
>
> Mwono hutegemea mambo mengi kiasi kwamba jitihada za kutokuwa na upendeleo hukosa maana. Kwa kutaja kwa uchache, mambo hayo ni: nafasi ya mtu kwa kuzingatia kiolwa, kukosekana kwa mwanga, umbali, maarifa ya awali, mtazamo wa kisaikolojia juu ya kiolwa; yote haya na mengine yanaathiri picha anayoitengeneza mwonaji na anavyoipeleka kwa wengine (Tafsiri yangu).

Uolezi, kwa mujibu wa Toolan (2001), unatekeleza majukumu mawili: mosi, kuwa kama chujio la taarifa, yaani kudhihirisha kiolwa fulani; na pili, kuwa kama dirisha ambalo kwalo msomaji anaweza kutazama matukio yanayotokea katika ulimwengu wa hadithi, yaani kubainisha mwono au itikadi ambayo kwayo kiolwa hicho kinatazamwa. Kutokana na dhima hizo ni bayana kuwa uolezi unahusu utambuzi ambao ni "mchakato wa kimwili na kiakili unaotegemea nafasi ya mtu anayeona..." (Bal, 2009:145). Kwa ujumla, kutokana na fasili ya dhana ya uolezi na maelezo mengine ni wazi kuwa uolezi una muolaji na kiolwa. Katika makala hii, uolezi katika matini umechunguzwa kwa kuzingatia mahali alipo muolaji.

### 3.1 Ujitokezaji wa Uolezi wa Jumla katika *Nagona* na *Mzingile*

Matukio katika riwaya hizi yanasimuliwa kwa kumtumia msimulizi nafsi ya kwanza ambaye anashiriki katika hadithi. Msimulizi huyu anawasilisha kile ambacho anafikiri na kukiona. Kwa hiyo, matukio, katika riwaya hizi, yanawasilishwa kwa mwono wa wahusika walio ndani ya simulizi; yaani anachokiona msomaji ni kile ambacho mhusika anakitambua au kile ambacho mhusika anakiona. Kwa maneno mengine, uolezi wa ndani umetumika kuwasilisha hadithi. Data zifuatazo zinabainisha uolezi huo wa ndani:

> Lakini nilijikuta nimechoka. Mbele yangu, niliona jiwe moja jeusi. Nilijikokota kwenda kulikalia. Kabla sijakaa nilisikia mtu akikohoa. Kwa hofu, nilisimama wima nikaangalia huku na huko. Hapakuwa na mtu. Nilikuwa wapi hapa! Nilitembea kwa harakaharaka kutoka hapo mahali. Nilianza kusikia sauti za watu wasomao vitabu. Kila mmoja alikuwa akisoma lake. Sikuona watu wala shule (Kezilahabi, uk. 1).
>
> Picha zilizoonyesha vituo vya njia ya msalaba zilikuwa bado zimening'inia kwenye nafasi zake. Nilitembea polepole hadi kule

> mbele. Haya ndiyo niliyoyaona: Macho yangu yalivutiwa mara moja na sanamu kubwa la Yesu msalabani ambalo halikuwa na kichwa. Niliposogea karibu, niliona kuwa kichwa kilikuwa kimedondoka chini. Kilikuwa na nyufa, lakini kilikuwa bado kimezungukwa na lile taji la miba. (Kezilahabi, kur. 96-97)

Katika dondoo la kwanza kutoka katika *Nagona*, msimulizi ambaye pia ni mhusika asiye na jina (anayejibainisha kwa kiambishi cha nafsi ya kwanza 'ni-' kurejelea kiwakilishi Mimi) ndiye anayeona jiwe na kusikia mtu anakohoa bila kuonekana. Kinachoolezwa katika dondoo hilo ni uajabuajabu wa mazingira aliyokuwamo muolaji mhusika, Mimi. Vifungu vya maneno kama "Kwa hofu", "Nilitembea harakaharaka" vinadokeza mashaka yaliyotokana na mazingira hayo ya uajabuajabu aliyokutana nayo katika safari yake. Aidha, katika dondoo la pili kutoka katika *Mzingile*, mhusika asiye na jina (naye anajibainisha kwa kiambishi cha nafsi ya kwanza 'ni-') ndiye muolaji. Miongoni mwa mambo yanayombainisha muolaji kuwa kauli yake ni "Haya ndiyo niliyoyaona..." Kauli hii inadhihirisha kuwa msimulizi anasimulia alichokiona yeye mwenyewe.

Katika madondoo yote hapo juu, muolaji ni mhusika nguli na msimulizi. Hata hivyo, kuna wakati Kezilahabi anatumia msimulizi nafsi ya kwanza katika kusimulia lakini muolaji anakuwa zaidi ya mmoja, akiwamo msimulizi. Mathalani, katika Kezilahabi (uk. 37) mwandishi anasema:

> Tulipoyakaribia majengo tulianza kushangaa. Majengo yalikuwa mazuri, lakini yote yalikuwa yamezungukwa na madimbwi ya maji machafu. Ilikuwa vigumu kuyafikia. Yalikuwa yamezungushiwa seng'enge na njia ya kuingia ilikuwa moja ambayo ilikuwa ikilindwa na askari mkondefu mwenye bunduki.

Dondoo hilo linaonesha anayesimulia ni msimulizi nafsi ya kwanza. Msimulizi huyu pia ni miongoni mwa waolaji. Kwa hiyo, msimulizi ni mmoja lakini waolaji wako zaidi ya mmoja. Waolaji hawa ni EGO, ID na SUPEREGO (uk. 31). Msomaji anatambua kuwa EGO, ID na SUPEREGO ndio waolaji kwa kurejelea nafsi ya wingi 'tu-' inayotumiwa na msimulizi nafsi ya kwanza. Kwa hiyo, msimulizi anaposema walianza kushangaa walipoyakaribia majengo ina maana kuwa EGO, ID na SUPEREGO, wote kwa pamoja, waliona majengo yale. Hivyo, kiolwa ni majengo mazuri yaliyozungukwa na madimbwi ya uchafu ambayo ni kiwanda kinachotengeneza baiskeli.

Uolezi tulioubainisha katika dondoo hapo juu unaonesha violwa kwa nje, yaani mwonekano wa nje wa violwa hivyo. Hata hivyo, uolezi unaweza kufanyika kwa muolaji kuonesha muonekano wa ndani wa violwa hususani uolezi unapolenga hisia na fikra. Kwa mfano:

> Nilianza kujiuliza moyoni, "Huyu msichana ni nani kwangu, na mimi ni nani kwake?" Nilikuwa na wazo lakini lilikataa kutoka...

> ... Sasa nilianza kuangalia alivyojengeka. Nilianza kutamanitamani. Kitu fulani kilikuwa bado kikitokea ndani mwangu. Nilianza kujiona mtu mzima tayari kushika madaraka na majukumu, "Je, nimekua?" nilijiuliza kimoyomoyo (Kezilahabi, uk. 64).

Aidha, katika *Mzingile* (uk. 32) uolezi wa fikra unajitokeza kama ifuatavyo:

> Karibu na altare niliona msalaba mmoja mkubwa. Nilitamani kufa kifo jasiri kama cha huyo jamaa. "Huyu bwana alikufa kishujaa na ndiyo maana akajenga msingi wa historia mpya!" nilisema kimoyomoyo. "Nitaijengaje historia?" nilijiuliza.

Katika dondoo kutoka *Nagona*, muolaji anataka msomaji aone kinachoendelea katika moyo wake, maswali na hisia zake. Katika mfano utokao katika *Mzingile* kiolwa ni fikra za muolaji kuhusu shujaa ni mtu wa aina gani. Katika fikra hizo anaonesha shauku yake ya kutaka kufa kwa ujasiri ili apate kuijenga historia. Kimsingi katika hali kama hii, muolaji pia ni kiolwa. Kutokana na uolezi wa mawazo na hisia, wasomaji wanapata fursa ya kutambua misukumo ya ndani ya wahusika na mitazamo yao kuhusu masuala mbalimbali.

Uolezi katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* ni ule wa mshuhudiaji aliye na ukomo na mwenye ufinyu wa maarifa kwa sababu ya muolaji kuwa mhusika katika hadithi. Aidha, ukomo wa muolaji katika riwaya hizi unatokana na yeye kutokuwa na uwezo wa kuona yanayoendelea kwingine isipokuwa pale alipo. Ingewezekana muolaji kuona sehemu mbalimbali iwapo angekuwa katika sehemu fulani ya juu ya ulimwengu wa hadithi.

### 3.2 Utambulisho wa Wahusika kupitia Uolezi: Paa na Mzee

Uolezi katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* umejitokeza kwa namna mbalimbali. Kama tulivyoeleza katika utangulizi, uolezi tunaouzingatia katika makala hii ni ule unaojenga utambulisho wa wahusika, 'Paa' katika *Nagona* na 'Mzee' katika *Mzingile*. Katika kujenga utambulisho na kusawiri mtazamo wa mwandishi dokezi, Kezilahabi anatumia waolaji wa ndani tofautitofauti ambao wanatambua violwa mbalimbali. Utambuzi huo unategemea nafasi aliyopo mtu ukihusisha na kiolwa, kukosekana kwa mwanga, umbali, maarifa aliyonayo muolaji, mtazamo wa kisaikolojia wa mwolaji juu ya kiolwa (Bal, 2009). Ujenzi wa utambulisho wa wahusika 'Paa' na 'Mzee' umejidhihirisha kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo:

#### 3.2.1 Ujenzi wa Utambulisho kupitia Uolezi wa Mazingira ya Wahusika

Mazingira, katika muktadha wa makala hii, yanahusisha mambo yamzungukayo mhusika, mathalani, chumba, nyumba, mtaa au mji pamoja na mazingira yake ya kijamii kama vile familia na tabaka lake kijamii (Rimmon-Kenan, 2002). Mwandishi dokezi amejenga utambulisho wa wahusika hawa na mtazamo kuhusu wao kupitia uolezi unaojidhirisha kwa kuolezwa violwa vya nje, mathalani, jengo

alilokuwa akiishi 'Paa'. Katika *Nagona*, nguli wa riwaya, akiwa na Nabii, Mtume, Mfuasi, na Mtenzi, anaonekana yuko katika safari ya kumtafuta 'Paa', safari iliyowafikisha katika jumba kubwa jeupe ambalo anapatikana 'Paa'. Jengo hilo linaelezwa namna hii:

> Kwa mbali tuliona jumba kubwa jeupe. Nyuma yake kulikuwa na mlima mkubwa ambao pia ulikuwa mweupe nchani. Tulitembea kuelekea ngome hiyo. Jengo lilikuwa limezungukwa na ukuta wa mawe wenye upana kiasi cha yadi moja. Ukuta ulikuwa mrefu. Juu ya ukuta huu palikuwa pamechomekewa mikuki ncha juu. Juu ya ncha hizi paliwaka ndimi za moto. Jengo zima likawa kama limezungushiwa mishumaa iwakayo (Kezilahabi, kur. 51-52).

Aidha Mzee, mhusika katika *Mzingile*, anaolwa kupitia mazingira ambayo kwayo nyumba yake ilijengwa. Inaelezwa:

> Nyumba hii ilikuwa imejengwa juu ya mwamba mmoja mkubwa. Mwamba huu ulikuwa juu ya mawe mengine makubwa. Ilikuwa vigumu kuufikia. Kichaa pekee angeweza kujenga mahali hapo. Si mtu wa akili timamu! Ilikuwa vigumu kujua aliyelala au kukaa humo alipanda na kushuka namna gani. Nilipumzika kwa muda wa siku mbili. Nilifikiria namna ya kuifikia nyumba hiyo ambayo haikuonyesha kuwa na dirisha. Wakati wote sikuona mlango unafunguliwa au mtu kutoka na kuingia ndani. Ilikuwa asubuhi nilipoanza jitihada ya kufika kwenye kilele (Kezilahabi, uk. 17).

Katika dondoo la awali, waolaji wa ndani, yaani Mimi, Nabii, Mtume, Mfuasi na Mtenzi, ndio wanaoona jengo. Kwa hiyo, jengo lilikuwa ndio kiolwa. Waolaji hao wanamtaka msomaji aone mwonekano wa nje wa kiolwa husika. Wanachotaka msomaji akione ni mazingira anayoishi 'Paa', mazingira yenye ngome na ulinzi mkali. Uolezi huu unajenga mtazamo kuwa 'Paa' anayetafutwa hapatikani kwa urahisi na kwamba unahitajika ujasiri ili kumpata. Aidha, inaolezwa kuwa mazingira aishiyo 'Paa' si ya giza kutokana na jengo kuwa jeupe na kuzungukwa na mishale iwakayo mithili ya mishumaa. Uolezi wa jumba hilo unajenga sifa inayomtambulisha 'Paa' ya kutopatikana kwa urahisi. Aidha, katika dondoo la pili kutoka katika riwaya ya *Mzingile*, muolaji, ambaye naye ni mhusika asiye na jina (anayejibainisha kwa kiambishi cha nafsi ya kwanza 'ni-' kurejelea kiwakilishi Mimi), anaona nyumba. Kwa kadiri ya utambuzi wake, ni nyumba ambayo si rahisi kufikika kutokana na kujengwa juu ya mwamba uliokuwa juu ya mawe makubwa. Pia, nyumba hiyo haina madirisha na wakati wote mlango umefungwa. Nyumba hii ilikuwa ya Mzee. Katika kuioleza namna hii, kupitia muolaji wa ndani mhusika, mwandishi dokezi anajenga ufahamu fulani kwa msomaji kuhusu Mzee anayeishi humo kuwa hafikiki kwa urahisi. Zaidi ya kujenga ufahamu huo, muolaji anajenga utambulisho wa Mzee kwa kuonesha uwezo wake ambao ni vigumu

kuulinganisha na mtu mwingine. Kwa hiyo, katika dondoo hilo muolaji ni nguli wa riwaya, Mimi, na kiolwa ni nyumba isiyofikika kwa urahisi.

Aidha, uolezi wa mazingira unajenga utambulisho wa Mzee katika *Mzingile* pale ambapo muolaji wa ndani aliye mhusika anatambua hali ya ndani ya nyumba ya Mzee huyo. Mwandishi dokezi ameandika:

> Nilisikia kiberiti kikiwashwa. Kisha, taa iliyotoa mwanga hafifu iliwaka. Kati yangu na yeye palikuwa na pazia la gunia kuukuu lililofanya nyumba igawanyike sehemu mbili. Nyuma ya gunia hili bovu niliona kiwiliwili cha mtu akijitahidi kujifunga blanketi kiunoni (uk. 19).
>
> Alisema haya akijikokota kwenda kwenye kochi la pili lililokuwa likitazamana na lile nililokalia. Alilokalia lilikuwa kuukuu zaidi (uk. 20).

Katika dondoo hilo, muolaji ni mhusika katika riwaya husika. Kiolwa ni mazingira ya ndani ya nyumba ya Mzee. Inaelezwa kuwa katika nyumba hiyo, kilichotenga kati ya sebule na chumba cha kulala ni pazia la gunia lililo kuukuu. Pazia hilo, zaidi ya kuwa kuukuu, ni gunia bovu. Ubovu wa pazia hilo la gunia umesababisha muolaji atambue kuwa nyuma ya pazia hili kulikuwa na kiwiliwili cha mtu anayejitahidi kujifunga blanketi. Zaidi ya pazia, katika dondoo linalotoka ukurasa wa 20, msomaji anatazamishwa samani kuukuu kama vile makochi. Muolaji mhusika anataka msomaji aole hali ya makochi hayo ili apate picha fulani kuhusu Mzee huyo. Kimsingi, mazingira haya yanayoolezwa na muolaji yanamfanya msomaji aone au atambue tabaka la Mzee. Kwa kuzingatia uolezi huo, mwandishi dokezi anamtumia muolaji wa ndani aliye mhusika kujenga utambulisho wa umaskini. Aidha, katika kujenga utambulisho huo, uolezi, katika dondoo hilo, umetumika kujenga mtazamo juu ya Mzee kuwa ni mtu fakiri asiye na msaada wowote. Chambilecho Madumulla (2009:55-56) kuhusu Mzee huyu anayemuita kimungu:

> Katika *Mzingile* mhusika mkuu anapitishwa katika wakati na mahali ambapo pamechakazwa na kudhoofishwa na kimungu kikongwe, tena kichovu, ambacho hakiishi kukimbia mafichoni kwa hofu ya kutimiza wajibu kilicho nao ambao umekizidi kimo, kwa hiyo kimeshindwa kuudhibiti. Kimungu hiki kinaelekea kuwa ni zao la mwanadamu aliyekata matumaini na aliyejaa kutofanikiwa na ukatili. Anguko la kimungu ni sawa na kufikia kitovu cha duara, ambacho ni kilele.

Kinachoelezwa na Madumulla kuhusu Mzee huyu, ambaye amesawiriwa kama kimungu, ni mhusika huyo kutokuwa na msaada wowote. Kutoweza kuwa na msaada wowote kunachangiwa na umaskini wa Mzee huyo unaoshuhudiwa na muolaji wa ndani aliye mhusika. Iwapo Mzee huyo anayedhaniwa kuwa na msaada mkubwa yuko katika hali hiyo ya umaskini, anawezaje kuwasaidia

wanaomtumainia? Kwa hiyo, utambulisho unaojengwa kupitia mwono wa muolaji unathibitisha hoja ya Madumulla kuhusu Mzee.

### 3.2.2 Ujenzi wa Utambulisho kupitia Uolezi wa Mwonekano wa Wahusika

Utambulisho wa wahusika, Paa katika *Nagona* na Mzee katika *Mzingile*, na mtazamo wa mwandishi dokezi juu ya wahusika hao umejengwa kupitia uolezi wa mwonekano wa wahusika hao ambao ndio violwa. Mwonekano huo wa wahusika umeolezwa kwa namna tofautitofauti. Katika *Nagona* mwandishi dokezi anawatumia wahusika mbalimbali ambao wanamtazama 'Paa' kwa namna tofauti na hivyo kusawiri mitazamo ya kijamii kuhusu dhana zinazowakilishwa naye pamoja na kudokeza utambulisho wa mhusika huyo. Mathalani, mwonekano wa Paa umeolezwa kama ifuatavyo:

> Nilisogea mbele polepole. Nilimfunua paa kuanzia kichwani hadi miguuni. Alikuwa msichana mzuri ambaye hajapata kuonekana. Nilipomfunua tu muziki ulilia. Aliposimama muziki uliacha (uk. 60).
>
> Naye pia alikuwa amekaa pembezoni mwa kitanda chake uchi, isipokuwa bunda la shanga lililozunguka kiunoni mwake. Akiwa amejipaka mafuta, mwili wake uling'aa ulipokutana na mwanga wa mshumaa. Tulitazamana tukihema. Mimi ndiye nilikuwa wa kwanza kusimama na kutembea kuelekea kitandani kwake (uk. 66).
>
> Nilitazama alikokuwa amesimama. Niliona mwili wake unaanza kutoa mwanga. Mwanga uliongezeka ukamulika kibanda kizima. Uzuri wake uliongezeka maradufu, halafu sauti yake ikasikika (uk. 67).

Madondoo hayo yanaonesha muolaji wa ndani aliye mhusika akimtazamisha msomaji mhusika Paa. Katika madondoo hayo, muolaji wa ndani ambaye pia ni mhusika anamuelekeza msomaji atazame mwonekano wa nje wa mhusika huyo. Katika dondoo la kwanza kutoka uk. 60, muolaji ambaye ni mhusika anamtaka msomaji aone kuwa Paa yule ni msichana mzuri. Aidha, katika dondoo linalotoka uk. 66, muolaji wa ndani mhusika anamuelekeza msomaji atazame hali ya msichana huyo, yaani paa, anapokuwa uchi. Katika hali hiyo, msomaji anatazamishwa mng'ao wa mwili wa paa. Mng'ao wa mwili huo unaelezwa kusababisha mwanga unaomulika kibanda kizima (tazama dondoo kutoka uk. 67 wa *Nagona*). Kimsingi muolaji wa ndani mhusika anamuonesha msomaji mvuto wa Paa, msichana, mvuto ambao umesababisha muolaji apate matamanio na hata kuchukua hatua ya kumsogelea pale kitandani (uk. 66). Muolaji huyu, ambaye ni mhusika na nguli wa riwaya, ndiye anamfanya msomaji amtazame "Paa" kuliko vitu au mambo mengine yaliyowazunguka kwa kuzingatia mtazamo wake. Mhusika nguli, ambaye pia ni muolaji, anawasilisha mtazamo wake kiitikadi "kupitia namna yake ya kuutazama ulimwengu" (Rimmon-Kenan, 2002:84), kwa kudhihirisha mtazamo huo kwa namna anavyomwonesha msomaji sifa za uzuri na mvuto wa "Paa". Kwa muolaji ambaye pia ni mhusika nguli, Paa ni mzuri na

mwenye mvuto kiasi cha kuleta matamanio ya kumsaka. Mtazamo huu umetokana na mahali alipo muolaji kwa kuzingatia kiolwa, maarifa ya awali kuhusu paa (rejea mazungumzo ya muolaji ambaye pia ni nguli wa riwaya na babu yake (kur. 73-84), na mtazamo wa kisaikolojia juu ya kiolwa.

Zaidi ya uolezi wa mwonekano wa Paa katika *Nagona*, pia kuna uolezi wa mwonekano wa Mzee katika *Mzingile*. Uolezi huo umejitokeza kama ifuatavyo:

> Juu ya kitanda alikuwa amelala mzee mmoja mwenye mvi nyingi. Alikuwa amejifunika blanketi kuukuu sana. Blanketi hilo lilikuwa na mashimo mengi yaliyoonyesha sehemu fulafulani za mwili wake. Macho yake yalikuwa yamefumba, lakini kupanda na kushuka kwa kifua chake kulinijulisha kuwa alikuwa bado hai. Niliitazama sura yake. Alifanana sana na baba yangu. Kumbe kadiri nilivyokua ndivyo nilivyozidi kufafanana naye (uk. 103).

Katika dondoo hapo juu msimulizi anasimulia kile ambacho aliona. Katika simulizi yake, alimuona mzee mwenye mvi nyingi akiwa amelala huku amejifunika blanketi. Blanketi hilo lilikuwa kuukuu sana kiasi cha kuwa na mashimo mengi. Kadiri simulizi yake inavyoendelea, anaonesha kuwa aliiona sura ya Mzee ambayo ilimfanya Mzee huyo afanane sana na baba yake msimulizi na muolaji. Msimulizi na muolaji huyu anamuonesha msomaji kuwa hata yeye, muoloji, anafanana na Mzee huyo. Katika dondoo hilo, zaidi ya kuolezwa kwa hali ya Mzee, mnaolezwa mwonekano wake kuwa alikuwa "mwenye mvi nyingi" na "sura ambayo ilifanana na baba yake muolaji". Uolezi wa mwonekano wa mvi nyingi unajenga utambulisho wa uzee na pengine hekima, na ule wa sura inayofanana na muolaji inamtambulisha Mzee kuwa mtu awezaye kufanana na yeyote hata kufikia kudhaniwa kwake kuwa baba. Hali hii ya nguli kumfananisha Mzee na baba yake na kisha naye kujiona anafanana na Mzee inadokeza uwezo wa Mzee kufanana na kila mtu. Utambulisho huu unamjenga Mzee kuwa Mungu, jambo ambalo linadhihirishwa na Mzee mwenyewe anaposema: "... Bado naukumbuka wakati wangu wa ujana. Wakati huo nilikuwa na sifa za kila aina. Wengine walinipa sifa ya *Omnipotentia*, wengine *Omniscientia*" (uk. 23). Dhana za *Omnipotentia* na *Omniscientia* zinarejelea sifa za Mungu. *Omnipotentia* inarejelea mamlaka au uwezo wote na usio na kikomo wakati *Omniscientia* inarejelea maarifa yote. Kwa hiyo, sifa hizi zinambainisha Mzee kuwa anaweza yote na anajua yote na hivyo kumsawiri kama Mungu. Kimsingi, kauli hizo za Mzee zinamuelekeza msomaji aole sababu za mazoea ya nguli wa riwaya ya kumfuatafuata Mzee hata kufikia hatua ya kuvunja milango ya nyumba ya Mzee mara kadhaa. Uvunjaji wa milango hii unatokana na kile anachokisema Mzee kuwa Mimi, ambaye ni nguli wa riwaya, anachanganya kuwako kwake na kuwako kwa Mzee na hata kufikia hatua ya kuanza kujinasibisha na Mzee huyo kwa kurudi nyuma kwa babu na babu hata kumfikia yeye (kur. 103-104). Kwa hiyo, mwonekano wa mvi nyingi na sura inayofanana na baba wa Mimi, nguli wa

riwaya, pamoja na kuhusishwa na mababu unamtambulisha Mzee kuwa Mungu kwa kuwa inaelezwa kuwa Mungu ni baba; na kama ni baba basi anafanana na kila mtu.

### 3.2.3 Ujenzi wa Utambulisho kupitia Uolezi wa Fikra za Wahusika wengine

Majukumu ya uolezi, kama yanavyotajwa na Toolan (2001), ni kudhihirisha kiolwa fulani pamoja na kuwa dirisha ambalo kwalo msomaji anaweza kutazama matukio yanayotukia katika ulimwengu wa hadithi. Kwa hiyo, uolezi, kwa mujibu wa Toolan, unaweka wazi kile kinachotazamwa pamoja na kuwa zana inayotumika kutazamia yanayoendelea hadithini. Katika jukumu la kudhihirisha kiolwa, yaani kile kinachotazamwa, mwandishi dokezi anaweza kumtumia muolaji ili kumfanya msomaji atazame fikra za wahusika kuhusu jambo fulani kwa lengo la kuweka wazi mtazamo juu ya suala husika. Uolezi wa fikra za wahusika mbalimbali kuhusu wahusika Paa na Mzee katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* kimtawalia, umesaidia kubainisha namna wahusika hawa, Paa na Mzee, wanavyotazamwa na hivyo kujenga utambulisho wao. Mathalani, katika *Nagona*, mmeolezwa fikra mbalimbali za wahusika juu ya mhusika Paa kama ifuatavyo:

> "Utamwona, na utakapomwona utashangaa kwa nini ulikuwa humwoni maana daima yu karibu nawe. Muhimu ni kufikiri, utashi na nia. Lakini kwa nini nikueleze haya yote wakati mimi mwenyewe nimeshindwa kumweka mikononi hadi ukingoni..."
>
> "Nagona ni mwanga. Ni kama jua lililopatwa na mwezi. Ukitazama kwa muda mrefu unaweza ukapofuka na usione chochote wakati wote wa uhai wako..." (uk. 80).

Dondoo hilo linaonesha kauli za babu yake nguli wa riwaya. Kauli hizo alizitoa katika mazungumzo yake na mjukuu wake ambaye ni nguli wa riwaya. Katika dondoo hilo muolaji wa ndani ambaye pia ni mhusika anaoleza fikra zake kuwa Nagona, ambaye ndiye Paa, ni mwanga unaoweza kumpofusha mtu autazamapo muda mrefu. Swali ambalo msomaji anaweza kujiuliza ni hili: Paa ni nani au nini hasa ikiwa katika riwaya hii muolaji mhusika anamuona kama mwanamke mzuri na hapa anaonwa kama mwanga? Bila shaka, kwa kuolwa namna hii, mwandishi dokezi anajenga mtazamo kuwa paa ni kitu cha thamani sana. Kupitia mtazamo huu tunaweza kusema kuwa paa anatambulishwa kama kitu kiondoacho giza. Giza liondokapo, mambo yanakuwa nuruni. Hakuna lililofichika. Uolezi huu wa paa kama mwanga na kupatikana kwake kwa kufikiri unaipa uzito hoja ya Diegner (2005) kuwa Paa ni ujuzi na ukweli. Ujuzi ambao kimsingi ni maarifa hufikiwa kutokana na tafakuri na hatimaye maarifa hayo huchukuliwa kuwa ndio ukweli wenyewe.

Aidha, katika *Mzingil*e mwandishi dokezi amewatumia waolaji wa ndani ili kuoleza fikra zao kuhusu mhusika Mzee, fikra ambazo zinatokana na mitazamo yao. Uolezi huo umejitokeza kama ifuatavyo:

> "Zamani, ndiyo. Lakini siku hizi mkali kidogo kwetu. Anasema tumemzoea vibaya. Tumefanya mahali pake kuwa kwetu. Hivyo ndivyo anavyonung'unika. Lakini nafikiri umri pia unaanza kumwelemea. Ukimsogelea tu anasema unammalizia hewa au unataka kumnyang'anya chakula chake."
>
> "Yaelekea hata mimi atanifukuza."
>
> "Hajawahi kumfukuza mtu yeyote. Ni mtu mzuri sana. Mfadhili atafukuzaje wenye shida ya haki? Wewe mwenyewe utamwona" (uk. 54).

Dondoo hilo linahusu mazungumzo baina ya Mimi, nguli wa riwaya, na Kipofu. Katika mazungumzo hayo mwandishi dokezi, kupitia waolaji wa ndani walio wahusika, anamtaka msomaji aole fikra za wahusika kuhusu Mzee. Fikra za wahusika zinazoolezwa zinaonesha mtazamo wao kuhusu Mzee kuwa 'anaelemewa na umri', 'mfadhili na mwenye matendo ya haki'. Suala la kulemewa na umri, kuwa kwake mfadhili na kuwa kwake mwenye matendo ya haki ni mtazamo ambao mwandishi dokezi anataka tuuone kuhusu Mzee. Mtazamo huo unajenga utambulisho wa Mzee, utambulisho wa ukubwa, ufadhili na mwenye haki.

Zaidi ya fikra hizo zinazodokeza mitazamo tofauti kuhusu Mzee, mwandishi dokezi anatumia waolaji tofauti kama vile mhusika nguli, kipofu, kijana na mwanasayansi. Katika safari ya nguli ya kupeleka taarifa za msiba kwa Mzee kuhusu mwanawe anapokuwa anarudi anakutana na watu mbalimbali ambao katika mazungumzo wanaonesha fikra zao kuhusu Mzee. Mathalani, nguli anapokutana na kijana, kijana anamuona Mzee kama mwenye uwezo wote (uk. 81); mwanasayansi anamuona Mzee kuwa anapatikana mahali kote (uk. 85) na kwamba ana uwezo wa kudhibiti fikra zao (uk. 93); na nguli anapomkuta Mzee nyumbani kwake baada ya kutoka safarini anamuita baba (uk. 103). Hawa wote ni waolaji wa ndani na ambao wanamuona Mzee kwa namna tofautitofauti. Mitazamo yao inategemea na kila mmoja mazingira yake na kwa hiyo, kinaratolojia, uolezi kuwa msambao, yaani "uwasilishaji wa jambo au tukio lilelile kama linavyotazamwa kupitia macho tofauti ya waolaji wa ndani" (Yannicopoulou, 2010:71). Fikra hizo za wahusika zinazoolezwa na mwandishi dokezi kupitia waolaji wa ndani zinadokeza utambulisho wa uungu wa Mzee. Utambulisho huu wa uungu umeolezwa kwa kutumia fikra tofautitofauti ili kusawiri mitazamo ya jamii juu ya Mungu. Kwa hiyo, mwandishi dokezi, kwa kumtumia muolaji, hulenga msomaji ayatazame mambo kwa namna yanavyotazamwa na muolaji kwa lengo la kujenga uelewa fulani. Mtazamo wa jamii au mtu yeyote unatokana na kuona. Mtu au jamii inapoona huchukua mtazamo fulani. Wazo hili linaelezwa vizuri na Kress na van Leeuwen (2006:163) ambao wanasema:

> *Seeing has, in our culture, become synonymous with understanding. We 'look' at problem. We 'see' the point. We adopt a 'viewpoint'. We 'focus' on an issue. We 'see things in perspective.' The world 'as we see it' (rather than 'as we know it' and certainly not 'as we hear it' or 'as we feel it') has become the measure for what is 'real' and 'true'.*

> Kuona, katika utamaduni wetu, kumekuwa na maana sawa na umaizi. Tunalitazama tatizo. Tunaona kiini. Tunachukua mtazamo fulani. Tunalenga hoja. Tunaona mambo kwa mwelekeo fulani. Ulimwengu kama tunavyoouona (badala ya 'kama tunavyoujua', 'tunavyoousikia' au 'tunavyouhisi') umekuwa kipimo cha nini kilicho halisi na nini kilicho kweli (Tafsiri yangu).

Suala hili la utambulisho wa uungu wa Mzee linatiliwa mkazo zaidi na mazungumzo ya Mwanasayansi na Mimi, nguli wa riwaya, hususani pale mwandishi dokezi anapomtumia muolaji wa ndani mhusika kumtazamisha msomaji fikra zake juu ya Mzee. Katika uk. 93 wa *Mzingile* inasimuliwa:

> "Tegemea kukuta mabadiliko makubwa. Baa la njaa na uharibifu uliotokea vimeweka nukta kwenye fikra ziutazamazo wakati kama mstari mmoja mrefu wenye mwanzo na mwisho. Sura yenye mtazamo mpya lazima ianze. Lakini nionavyo mimi, sura hii mpya haiwezi kuanza hadi Mzee atakapoondoka katika kitovu cha duara. Lazima aache kuzuru mashamba ya fikra zetu, japokuwa inasemekana anao uwezo wa kurutubisha".

Hapa mwandishi dokezi anataka msomaji aole, kupitia muolaji wa ndani, athari za uharibifu katika kufikiri. Aidha, msomaji anatazamishwa fikra za mwanasayansi ambaye ni muolaji wa ndani, kuhusu Mzee kuwa yeye ndiye kikwazo cha mwanadamu kujikwamua. Kwa msingi huo, kwa sababu ya Mzee, mwanadamu hana uhuru wa kufikiri kwa sababu huingiliwa na fikra za Mzee. Fikra za mwanasayansi kuwa Mzee ndiye kikwazo cha mwanadamu kujikwamua zinathibitishwa na mazungumzo ya nguli na Mzee kama ifuatavyo:

> "Mwongo mkubwa! Kila mahali niendako nakukuta! Wewe ndiye uliyenifanyia mazingaombwe niwe mtu wa kukufuata wewe milele! Mimi si mtumwa wako. Nataka uhuru wangu sasa..."

> "Mwongo ni wewe na wote wa aina yako! Tazama! Mimi ndiye ninayetaka uhuru toka kwako. Kila ninakohamia unanifuata. Unaninyima muda wa faragha!... Unanitafuta kanisani, msikitini, makaburini, mbuyuni, na hata ndani ya magofu! Shida yako nini kama siyo umbea unaoutafuta?"

> "Wewe ndiye unayestahihili lawama. Huna shukrani! Ukiniambia fanya hili, ninafanya. Lala chini, ninalala. Abudu, ninaabudu. Zunguka kama pia, ninazunguka. Umenifanya kikaragosi chako hatautu wenyewe sina tena..." (uk. 104).

Katika dondoo hilo, msomaji anaelekezwa aole sababu za mwanadamu kutokuwa huru. Sababu kubwa inayotajwa ni kuwapo kwa Mzee ambaye amekuwa akiwashurutisha watu kutenda mambo mbalimbali. Aidha, Mzee, ambaye kimsingi ni Kimungu kama asemavyo Madumulla (2009), anamuelekeza msomaji aole kuwa utumwa wa nguli unatokana na kiherehere chake cha kumfuatafuata Mzee. Kwa hiyo, utambulisho unaoendelea kujengwa hapa ni uungu wa Mzee.

## 3.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza uolezi katika riwaya mbili za Euphrase Kezilahabi za *Nagona* (1990; 2011) na *Mzingile* (1991; 2011). Katika kuchunguza suala hilo, makala imechambua namna uolezi ulivyotumika kujenga utambulisho wa wahusika, Paa katika *Nagona* na Mzee katika *Mzingile*. Uchambuzi umeonesha kuwa wahusika, Paa na Mzee, wamejengwa kupitia uolezi wa mazingira yanayowazunguka, mwonekano wao pamoja na fikra za wahusika wengine. Aidha, uolezi wa fikra za wahusika wengine umebainisha mwono au itikadi ambayo kwayo kiolwa kinatazamwa. Mathalani, uolezi wa fikra za nguli wa riwaya ya Mzingile kuhusu Mzee umedokeza mitazamo mbalimbali kuhusu Mzee huyo, ambaye Madumulla (2009) anamwita 'kimungu'. Kwa muhtasari, katika uchambuzi wa jumla wa riwaya hizi, imebainika kuwa, kunajitokeza uolezi wa ndani kutokana na waolaji kuwa wahusika. Aidha, imebainisha kuwa uolezi, zaidi ya kuwa mbinu ya kujenga mtazamo ki-Naratolojia, pia umetumika kujenga utambulisho wa wahusika katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*.

## Marejeleo


Bal, M. (2009). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative* (Toleo la 3). Toronto: University of Toronto Press.

Diegner, L. (2005). "Intertextuality in the Contemporary Swahili Novel: Euphrase Kezilahabi's *Nagona* na William Mkufya's *Ziraili na Zirani*". *Swahili Forum.* Juz. 12: 25-35. Inapatikana katika https://ul.qucosa.de/api /qucosa%3A11512/attachment/ATT-0/. Ilisomwa tarehe 15 Desemba 2021.

Flavian, L. (2021). Uchambuzi wa Mbinu za Kisimulizi Katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi. Tazimili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay in Method*. Mfasiri J.E. Lewis. New York: Cornell University Press.

Jahn, M. (1996). "Windows of Focalization: Deconstructing and Reconstructing a Narratological Concept." *Style*. Juz. 30(2): 241-267.

Kezilahabi, E. ([1990] 2011). *Mzingile*.Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Kezilahabi, E. ([1991] 2011). *Nagona*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Kress, G. na van Leeuwen, T. (2006). *Reading Images: The Grammar of Visual Design* (Toleo la pili). London: Routledge.

Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Nelles, W. (1990). "Getting Focalization into Focus". *Poetics Today*. Juz. 11(2): 365-382. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/pdf/1772622.pdf. Ilisomwa 21 Septemba 2021.

Parker, R.D. (2015). *How to Interpret Literature: Critical Theory for Literary and Cultural Studies* (3rd edition). New York: Oxford University Press.

Rimmon-Kenan, S. (2002). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics* (Toleo la pili). London: Routledge.

Wafula, M.N. (2011). "'Tradition' versus 'Modernity': Generational Conflict in *Vuta N'kuvute*, *Kufa Kuzikana*, *Msimu wa Vipepeo* and *Tumaini*." *Swahili Forum.* Juz. 18: 135-162.

Yannicopoulou, A. (2010). "Focalization in Children's Picture Books: Who See in Words and Pictures?" Katika Cadden, M. (Mh.), *Telling Children's Stories: Narrative Theory and Children's Literature*. Lincoln: University of Nebraska Press. Kur. 65-84.